JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
……..
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA
(Barua zote ziandikwekwaMkurugenziMtendaji)

Simu: 028 2226016,
Nukushi: 028 2226152,
pepe: ded.ngara@kagera.go.tz
ded@ngaradc.go.tz

si ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L. P. 30,
NGARA Barua

Kumb.Na.NGR/DC/CD/GNR/06/132
27/06/2018

YAH: HALI HALISI YA MIKOPO ILIYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA UZALISHAJI MALI VYA VIJANA NA WANAWAKE KWA ASILIMIA 10% YA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI KWA MWAKA 2014/2015 HADI 2017/2018.

Halmashauri ya wilaya ya Ngara imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali vya vijana (YDF) na wanawake (WDF) kwa kutumia asilimia 10% ya makusanyo ya ndani ili waweze kujikwamua kiuchumi na kijamii na kuondokana na umasikini uliokithiri miongoni mwa jamii.

Kwa mwaka 2014/2015, Halmashauri ilichangia kiasi cha T.shs. 1,000,000/= na kiasi cha T.shs. 8,000,000/= kilitoka wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto na kukopesha jumla ya vikundi 7 vya wanawake.

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hakuna mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya vijana na wanawake kutokana na mapato ya ndani ya halmashauri kuwa chini sana na kushindwa kukidhi mahitaji.

Kwa mwaka 2016/2017, Halmashauri ilikadiria kukusanya kiasi cha T.shs. 1,641,275,300/= kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani na makadirio ya kutoa kiasi cha T.shs. 164,127,530/= asilimia 10% ya mikopo ya vijana na wanawake.
Makusanyo halisi jumla ilikuwa **T.shs. 1,025,126,193.51** ambapo asilimia 10% ya fedha hizo ni **T.shs. 102,512,619.35** na zilitolewa jumla ya **T.shs. 29,000,000.00** sawa na asilimia **28.3%** ya fedha iliyotakiwa kutolewa kwa vikundi vya uzalishaji mali vya vijana na wanawake.

Fedha hizo zilikopeshwa kwa vikundi 22, kati ya hivyo 09 vya wanawake vilikopeshwa T.shs. 11,500,000/= na vikundi 13 vya vijana vilikopeshwa T.shs. 17,500,000/=.

Kwa mwaka huu 2017/2018, makadirio ya makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka ilikuwa T.shs. 1,035,005,000/= na kutoa asilimia 10% ya T.shs. 103,500,500/= kwa vikundi vya wanawake na vijana.
Makusanyo halisi hadi Juni 30, 2018 ilikuwa T.shs. 930,708,085.20 ambapo asilimia 10% ni T.shs 93,070,808.52.
Mwezi Marchi, 2018, zilitolewa jumla ya **T.shs. 13,621,730**/= kwa vikundi 10, kati ya hivyo 05 vya vijana T.shs. 6,810,865.00 na vikundi 05 vya wanawake T.shs. 6,810,865.00 sawa na asilimia 16.8%.

Mwishoni mwa mwezi Juni, 2018, jumla ya vikundi 08, kati ya hivyo 02 vikundi vya vijana na 06 vikundi vya wanawake, vilipewa mkopo wa jumla ya **T.shs. 16,378,270/=. Kiasi cha T.shs. 5,000,000/= za vikundi vya vijana na T.shs. 11,378,270/=** za vikundi vya wanawake.
Hii inafanya kiasi cha fedha kilichotolewa kama mikopo ya vijana na wanawake kwa mwaka 2017/2018 kuwa **T.shs. 30,000,000/= ambazo ni sawa na asilimia 32.**2% ya fedha ambazo zilitakiwa kutolewa kutokana na mapato ya ndani ya halmashauri kwa mwaka 2017/2018.

<u>Changamoto za jumla.</u>
Aidha kumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo halmashauri inakumbana nazo katika shughuli za utoaji wa mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake, lakini zaidi ni kwa vikundi vya vijana kama ifuatavyo:-

i. Ufinyu wa bajeti na makusanyo ya halmashauri ambapo husababisha kutofanyika kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa vikundi vilivyopewa mikopo kwaajili ya kutoa ushauri na kuhamasisha kurejesha mikopo katika muda uliopangwa ili vikundi vingine viweze kukopa fedha hizo.

ii. Ufinyu wa mapato ya ndani ya halmashauri na shughuli nyingi zinazotegemea fedha hizo ikiwemo utengenezaji wa magari, ununuzi wa mashine za kukusanyia mapato (POS mashine) kutoka mashine 05 hadi 75 za sasa sawa na asilimia 100% ya mahitaji ya halmashauri , hii ilisababisha kutofikia asilimia ya malengo ya fedha zilizopangwa kutolewa za mikopo ya vijana na wanawake.

iii. Vijana walio wengi kuamua kugawana fedha za mikopo walizopewa kwa matumizi mengine na kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati na wakati mwingine kushindwa kabisa kurejesha hata kidogo.

iv. Baadhi ya wanavikundi kuhamia nje ya wilaya kwaajili ya utafutaji bila kurejesha mikopo waliyochukua.

Mikakati ya kukabiliana na changamoto:

i. Kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ya ndani ili kuongeza kipato na kuweza kutoa asilimia 10% ya mikopo ya vikundi vya vijana na wanawake kama itakavyokuwa imepangwa.

ii. Kuendelea kufanya ufuatiliaji kwa vikundi vya vijana na wanawake ambavyo vimechelewa kurejesha mikopo waliyopewa ili kuwezesha vikundi vingine kukopeshwa na kujikwamua kiuchumi.

iii. Kuomba kufanya marekebisho ya mkataba wa ukopeshaji wa vikundi ili kuongeza kipengele cha kuvichukulia hatua za kisheria vikundi ambavyo vitashindwa kurejesha mikopo waliyopewa kwa wakati. **(Mkataba huo kwa sasa hauelezi chochote).**

iv. Kuiomba serikali kuruhusu halmashauri kuongeza akaunti maalumu ambayo itakuwa ikitumika kutunza fedha za vikundi vya vijana, wanawake na walemavu. Hii itarahisisha shughuli nzima ya ukopeshaji.

Taarifa kamili ya mikopo na marejesho kwa vikundi vya wanawake na vijana vilivyopewa mikopo ya asilimia 10% kutokana na mapato ya ndani ya halmashauri imeambatishwa.

Naomba kuwasilisha.

Josephine J. Lusatira,
KAIMU AFISA MAENDELEO YA JAMII (W),
NGARA.